Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

# MAPENDEKEZO YA KUANZISHWA KWA MAMLAKA YA BIDHAA NA MIUNDOMBINU YA MIFUGO







## Utangulizi

- Tanzania ni nchi ya pili kwa idadi kubwa ya Mifugo barani Afrika baada ya Ethiopia
- Idadi ya ng'ombe ni **milioni 36.6**, mbuzi **milioni 26.6**, kondoo **milioni 9.1**, na kuku **milioni 97.9** (Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2023/24)
- Sekta ya Mifugo inachangia asilimia **7%** kwenye pato la taifa. Uchangiaji huu unatofautiana na mataifa mengine yenye mifugo michache kama vile **Nigeria: mll 21 (13%), Uganda: mil 14 (13%)** na **Kenya:mil 22 (12%)**
- Sekta ya mifugo inachangia kwenye lishe na kipato cha kaya. Takribani **53%** zinafuga kuku, **32%** zinafuga ng'ombe, **10%** nguruwe, **4%** mbuzi, na kondoo **1%**
- Mfumo wa Ufugaji nchini Tanzania kwa asilimia kubwa ni wa kiasili na unachangia katika kujikimu na kuingiza kipato cha kaya

| Aina ya Mifugo | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ng'ombe | 30,496,687 | 32,186,600 | 33,928,391 | 35,256,637 | 36,584,883 |
| Mbuzi | 18,847,657 | 20,000,000 | 24,568,396 | 25,574,446 | 26,580,497 |
| Kondoo | 5,345,468 | 5,535,468 | 8,516,990 | 8,802,462 | 9,087,935 |
| Nguruwe | 1,944,300 | 2,015,600 | 3,208,495 | 3,439,362 | 3,670,229 |
| Kuku | 74,755,000 | 79,134,500 | 87,659,580 | 92,799,956 | 97,940,332 |
| **Ukuaji wa sekta asilimia** | **5** | | | | |
| **Mchango kwenye Pato la Taifa asilimia** | **7** | | | | |
| **Uvunaji asilimia** | **10** | | | | |

*Ukuaji wa Sekta, Mchango kwenye pato la Taifa na uvunaji*

| Nchi | Ng'ombe (Milioni) | Kondoo na Mbuzi (Milioni) | Mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye Pato la Taifa |
|---|---|---|---|
| Ethiopia | 65 | 25 | 16 |
| Tanzania | 36.6 | 35.7 | 7 |
| Nigeria | 21 | 116 | 13 |
| Kenya | 22 | 46.6 | 12 |
| Uganda | 14 | 20.5 | 13 |
| DRC | 1.2 | 6 | Haipatikani |

*Uzalishaji na uchangiaji wa mifugo kikanda*

## DIRA NA DHIMA

***Dira***

Kuwa taasisi inayotambulika kitaifa na kimataifa inayobadilisha tasnia ya mifugo kuwa yenye faida, inayoendeshwa kwa ubora na kuchangia ipasavyo katika mfumo wa chakula

***Dhima***

Kuboresha mazingira wezeshi ya biashara ya mifugo na bidhaa zake yanayoambatana na miundombinu na udhibiti wenye ufanisi katika minyororo ya thamani ya mifugo na mazao yake

| MAADILI YA MSINGI | |
|---|---|
| ***Uwazi:*** | Uwazi katika utoaji wa huduma; |
| ***Uadilifu:*** | Maadili na uaminifu; |
| ***Kujali Wateja:*** | Kuweka mazingira rafiki na kukidhi matarajio ya wateja; |
| ***Huduma bora:*** | Kutimiza malengo tarajiwa kwa kuzingatia majukumu na wajibu wa Bodi; |
| ***Uwajibikaji:*** | Wajibu wa kutekeleza majukumu kwa mujibu wa sheria na kanuni; |
| ***Kutopendelea:*** | Utoaji wa huduma bila ubaguzi; na |
| ***Ushikiaono:*** | Kufanya kazi kwa pamoja ili kuongeza ufanisi. |

## MAPENDEKEZO YA KAZI ZA MAMLAKA

i. Kumshauri Waziri katika masuala yanayohusu sera na mikakati ya uendelezaji na udhibiti wa mazao na miundombinu ya mifugo;
ii. Kufanya kazi za maendeleo, uendelezaji na udhibiti katika miundombinu ya mifugo, mazao ya mifugo na mifugo;
iii. Kutafuta, kuendeleza na kusimamia masoko ya ndani, kikanda na kimataifa ya mifugo na mnyororo wa fhamani wa mazao ya mifugo;
iv. Kuandaa na kufuatilia mikakati na mipango iliyoundwa ili kufikia ufanisi katika minyororo ya thamani ya mifugo na mazao ya mifugo;
v. Kuandaa na kuwezesha utekelezaji wa mikakati ili kujitosheleza kwa mifugo na mazao yake Pamoja na utoshelevu wa miundombinu ya mifugo;
vi. Kuchambua na kushauri kuhusu mwenendo wa masoko ya mifugo na mazao yake ndani ya nchi, kikanda na kimataifa
vii. Kutambua, kukuza, kuratibu na kusimamia utafiti na ubunifu katika mifugo, bidhaa na miundombinu yake
viii. Kukuza na kuwezesha matumizi ya teknolojia ifaayo ili kuongeza ufanisi katika minyororo ya thamani ya mifugo, mazao ya mifugo na miundombinu ya mifugo;
ix. Kuunda na kukuza mazingira ya ushindani wa biashara katika mifugo, mazao ya mifugo na miundombinu ya mifugo;
x. Kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza takwimu na taarifa zinazohusiana na mifugo, mazao ya mifugo na miundombinu yake;
xi. Kukuza na kuwezesha uundaji wa vyama vya wadau au vyombo vingine vya wadau mifugo, mazao ya mifugo na miundombinu yake;

xii. Kusajili, kutoa leseni na vibali kwa wafanyabiashara wa mifugo, mazao ya mifugo na watengenezaji na waendeshaji miundombinu ya mifugo;
xiii. Kukuza na kujennga uwezo uwezo wadau wa mifugo, mazao ya mifugo na miundombinu ya mifugo
xiv. Kuweka na kutekeleza viwango vya minyororo ya thamani ya mifugo na mazao yake na miundombinu ya mifugo kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zinazohusika;
xv. Kukuza na kuwezesha uhamasishaji wa rasilimali za umma na binafsi kwa ajili ya uwekezaji katika minyororo ya thamani na miundombinu ya mifugo na mifugo;
xvi. Kukuza na kuwezesha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na aina nyingine za mashirikiano katika kuendeleza minyororo ya thamani ya mifugo na mazao ya mifugo na miundombinu ya mifugo; na
xvii. Kukuza uendelezaji au uanzishwaji wa hifadhi za kimkakati na zenye ufanisi za mazao ya mifugo


## MATOKEO YA KATI

- Kuboresha tija katika uzalishaji
- Kuongeza uvunaji wa mifugo
- Kupunguza kiwango cha vifo vya mifugo
- Kuboresha mchango wa sekta katika Pato la Taifa
- Kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna

## MATOKEO MAKUBWA

- Kuboresha usalama wa chakula
- Kuboresha ufanisi katika mfumo wa masoko
- Kuboresha uongezaji wa thamani
- Kuboresha uwekezaji wa sekta binafsi
- Kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi
- Kuboresha utambuzi na ufuatiliaji
- Kuboresha kipato cha wafugaji

## Muundo pendekezwa wa Mamlaka



## MFUMO WA KISHERIA

- Mamlaka ni chombo huru kinachoundwa na sheria chenye mamlaka au madhumuni maalum.
- Mamlaka mara nyingi huanzishwa ili kusimamia huduma za umma au vifaa vinavyohitaji utaalamu maalum au utawala uliojitolea.
- Kwa kawaida hufanya kazi kwa kiwango cha uhuru kutoka kwa wizara au idara ya serikali ambayo wanashirikiana nayo.
- Mamlaka zinaweza kuwa na uwezo wa kutunga kanuni, kukusanya ada au tozo, na kusimamia utekelezaji wa sera zinazohusiana na eneo lao la wajibu.
- Mamlaka mara nyingi huambatana na uwajibikaji kwa matokeo ya maamuzi au matendo

## Takwimu za Mifugo


Ng'ombe milioni **36.6**


Mbuzi milioni **26.6**


Kuku milioni **97.9**


Mbuzi milioni **9.1**


Minada ya Awali **504**


Minada ya Upili **14**



Masoko ya Mpakani **11**

## Takwimu za Miundombinu


Idadi ya Machinjio **2000**


Idadi ya majosho **2,513**


Idadi ya Mizani **86**

Idadi ya vituo vya kukusanyia Maziwa (Collection centers) **196**





Sehemu za kuhifadhia Mifugo **27**

**Mawasiliano:**
Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, S.L.P 2870, Mji wa Serikali Mtumba Dodoma, Tanzania
Barua pepe: barua@mifugo.go.tz

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE
ASPIRES Tanzania *Agricultural Sector Policy and Institutional Reforms Strengthening*
MICHIGAN STATE UNIVERSITY